

HALMASHAURI YA WILAYA YA SIKONGE.

MUHUTASARI WA KIKAO MAALUMU CHA BODI YA ZABUNI
KILICHOFANYIKA TAREHE 29/10/2021

MAHUDHURIO:

- | | |
|---------------------------|------------|
| 1. Bw. Geofrey M. Hamis | Mwenyekiti |
| 2. Bw. Shadrack T. Baruti | Katibu |
| 3. Bw. Hashim M. Kazoka | Mjumbe |
| 4. Bw. Paschal O. Kapinga | Mjumbe |
| 5. Bi. Anibariki Ngata | Mwalikwa |

SECRETARIET

1. Revocatus Shabani
2. Joviness John

MUHUT. Na. 01/10/2021 KUFUNGUA KIKAO

Mwenyekiti alifungua kikao saa 5.30 asubuhi kwa kuwakaribisha wajumbe katika kikao cha siku hiyo. Pia Mwenyekiti aliwakumbusha wajumbe kwamba kikao cha siku hiyo kilikuwa ni kikao maalumu hivyo agenda yake ni moja tu.

MUHT. Na. 02/10/2021 : KUSOMA NA KUTHIBITISHA AGENDA ZA KIKAO.

Wajumbe walisoma na kuthibitisha agenda za kikao maalumu cha siku hiyo ambacho kilikuwa na agenda zifuatazo:

1. Kufungua kikao.
2. Kusoma na kuthibitisha agenda za kikao
3. Kuidhinisha njia ya Manunuzi ya 'FORCE ACCOUNT' katika miradi ya UVICO 19
4. Mengineyo kwa idhini ya Mwenyekiti
5. Kufunga kikao.

MUHT. Na. 03/10/2021 : KUIDHINISHA NJIA YA MANUNUZI YA 'FORCE ACCOUNT' KATIKA MIRADI YA UVICO 19

Afisa Elimu wa Taaluma wa Sekondari aliwasilisha taarifa kwamba mnamo tarehe 21/10/2021 walipokea fedha toka Serikali kuu kwa ajili ya kugharamia ujenzi wa madarasa katika Shule mbali mbali za Msingi na Sekondari katika Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge. Mradi huu utatumia fedha za UVICO 19, hivyo Idara za Elimu Msingi na Sekondari zinapendekeza Bodi ya Zabuni iridhie njia ya manunuzi itakayotumika iwe ya 'FORCE ACCOUNT' kama mwongozo wa miradi hiyo unavyoelekeza. Shule zilizoteuliwa kupata Fedha za UVICO 19 ni kama ifuatavyo:

1. SHULE ZA MSINGI

S/NA	JINA LA SHULE / KITUO	IDADI YA MADARASA	KIASI KILICHODHINISHWA TSH.
1.	Shule Shikizi ya Mwakasembo	2	40,000,000.00
2.	Shule Shikizi ya Msisi	2	40,000,000.00
3.	Shule Shikizi ya Mapala	4	160,000,000.00
4.	Shule Shikizi ya Kiswahilini	2	40,000,000.00
5.	Shule Shikizi ya Uyega	3	60,000,000.00
6.	Shule Shikizi ya Mang'wina	5	100,000,000.00
7.	Shule Shikizi ya Gezaule	2	40,000,000.00
8.	Shule Shikizi ya Mwamalia	2	40,000,000.00
9.	Shule Shikizi ya Idimbwa	7	140,000,000.00
10.	Shule Shikizi ya Uswaga	6	120,000,000.00
	JUMLA KUU		780,000,000.00

2. SHULE ZA SEKONDARI

S/NA	JINA LA SHULE / KITUO	IDADI YA MADARASA	KIASI KILICHODHINISHWA TSH.
1.	Shule ya Sekondari Chabutwa	3	40,000,000.00
2.	Shule ya SEkondari Kilumbi	3	60,000,000.00
3.	Shule ya Sekondari Kiwere	4	80,000,000.00
4.	Shule ya Sekondari Klsanga	2	60,000,000.00
5.	Shule ya Sekondari Mole	4	80,000,000.00
6.	Shule ya Sekondari Igigwa	4	80,000,000.00
7.	Shule ya Sekondari Langwa	4	80,000,000.00
8.	Shule ya Sekondari Milbono	3	60,000,000.00
9.	Shule ya Sekondari Pangale	2	40,000,000.00
10.	Shule ya Sekondari Ngulu	4	80,000,000.00
11.	Shule ya Sekondari Kamagi	3	60,000,000.00
12.	Shule ya Sekondari Mpombwe	2	40,000,000.00
13.	Shule ya Sekondari Msuva	2	40,000,000.00
14.	Shule ya Sekondari Tutuo	4	80,000,000.00
15.	Shule ya Sekondari Usunga	2	40,000,000.00
16.	Shule ya Sekondari Ugunda	3	60,000,000.00
17.	Shule ya Sekondari Kipili	4	80,000,000.00
18.	Shule ya Sekondari Kiloli	4	80,000,000.00
19.	Shule ya Sekondari Mkolye	2	40,000,000.00
	JUMLA KUU		1,180,000,000.00

Wajumbe wa Bodi ya Zabuni walipokea taarifa na kuijadili na wakaidhinisha kwamba njia ya Manunuzi Itakayotumika katika ujenzi wa madarasa yanayojengwa kwa kutumia fedha za UVICO 19 ni njia ya 'FORCE ACCOUNT'

MUHUT. Na. 04/10/2021. MENGINEYO KWA IDHINI YA MWENYEKITI

Hapakuwepo na mengineyo

MUHUT. Na. 05/10/2021. KUFUNGA KIKAO

Mwenyekiti alifunga kikao saa 6.47 mchana

UMETHIBITISHWA

MWENYEKITI

KATIBU

SAHIHI.....

SAHIHI.....

TAREHE 29/10/2021